

# جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي مَشْرُوعُ تَعَلُّمِ الْإِسْلَامِ – أَحْكَامُ الصَّلَاةِ - سَوَاحِيلِي

## Samo la 2

## الدرس الثاني

### **MAMBO MUHIMU YANAYOFUNGAMANA NA SWALA, NI HAYA YAFUATAYO;**

1. Uwajibu wa kswali jamaa msikitini kwa wanaume kutokana na Hadithi ya Mtume (saw) anasema :

(( لقد هممت أن أمر بالصلاة فنتقام ، ثم أخالف إلى منازل قوم لا يشهدون الصلاة معنا فأحرق عليهم )) [متفق عليه: 2420 ، 651].  
(Ninania kuamrisha swala iswaliwe, kisha niondoke kwenda kwenye majumba ya watu ambao hawahudhuri swala msikitini nikayatie moto) (Ameipokea Bukhari na Muslim: 2420, 651).

2. Inatakiwa kwa muislamu kwenda msikitini mapema kwa utulivu na unyenyekevu.

3. Ni sunnah kwa yule mwenye kuingia msikitini atangulize mguu wa kulia, ataomba dua iliyopokelewa kwa mtume (saw) :

(( اللَّهُمَّ افْتَحْ لِي أَبْوَابَ رَحْمَتِكَ )) [رواه مسلم: 1652].

(Ewe mwenyezi mungu nakuomba unifungulie milango ya rehema zako) (Ameipokea Imam Muslim :1652).

4. Ni sunnah kuswali rakaa mbili tahiyat masjid (rakaa mbili za kusalia msikiti) kabla ya kukaa, kwa hadithi aliyopokea Abu Qatada (R.A):

قال رسول الله ﷺ: (( إذا دخل أحدكم المسجد ، فليركع ركعتين قبل أن يجلس )) [متفق عليه: 444 ، 714].  
(Atakapo ingia mmoja wenu Msikitini askae mpaka aswali rakaa mbili kabla ya kukaa) (Ameipokea Bukhar na Muslim : 444, 714).

5. Ni wajibu kujisitiri tupu mbili wakati wa kuswali, na tupu ya mwanamume ni kuanzia kitivuni mpaka magotini na tupu y mwanamke mwili wake wote ni uchi isipokuwa uso wake.

6. Ni wajibu kuelekea qibla, ni sharti la kukubaliwa swala. isipokuwa katika hali mbili;

A. Kupatikane kizuizi kutokana na maradhi na mfano wake, ikasababisha kutoweza kuelekea qibla.

B. Kwenye safari hali ya kuwa anakwenda hali hii ni hasa katika swala za sunnah sio swala za faradhi.

7. Ni wajibu kutekeleza swala kwa wakati wake, kwani haiswihi swala kuswaliwa kabla ya wakati wake na haramu kuichelewesha swala kutoka kwenye wakati wake.

8. Kuleta takbira kwenye swala, na kupapia safu ya kwanza, na kusubiria swala, kufanya hivyo kuna fadhila kubwa sana. Hadithi ya Abu Huraira :

قال رسول الله ﷺ: (( لو يعلم الناس ما في النداء والصف الأول ، ثم لم يجدوا إلا أن يستهموا عليه

لاستهموا ، ولو يعلمون ما في التهجير [ أي: التكبير] لاستبقوا إليه ... الحديث )) [متفق عليه: 615 ، 437].  
(Laiti watu wangelijua ubora wa adhana na swafu ya kwanza, kisha wasipatikane isipokuwa kwa kutoa kitu wangelitoa, na laiti watu wangelijua ubora wa takbira ya pamoja na Imamu wangeishindania...) (Ameipokea Bukhar na Muslim :615, 437).

قال ﷺ: (( لا يزال أحدكم في صلاة ما دامت الصلاة تحبسه... الحديث )) [رواه البخاري ومسلم: 659 - 649].  
(Hataacha kuwa mmoja wenu kwenye swala maadamu swala inamzuiya) (Ameipokea Bukhar na Muslim: 659, 649).